# Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (Jica) Nusu karne ya Ushirikiano katika kuendeleza Sekta ya Kilimo Tanzania



*Wakati wa uvunaji katika skimu ya Umwagiliaji ya Lower Moshi.*



*Muonekano wa soko na vituo vya uuzaji wa samaki vya Malindi mara baada ya kukamilika.*



*Muonekano wa soko na vituo vya uuzaji wa samaki vya Malindi mara baada ya kukamilika.*

Hapa nchini Tanzania, Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (JICA), imetekeleza mfululizo wa miradi ya ushirikiano iliyoanza mnamo mwaka 1974 kwa uundaji wa Mpango jumuishi wa Maendeleo wa Kilimanjaro "Kilimanjaro Region Integrated Development Plan". Baada ya hapo, miradi ya maendeleo kama vile "Mradi wa Umwagiliaji wa Lower Moshi ikifuatiwa na "Kituo cha Kuendeleza Kilimo Kilimanjaro" "Kilimanjaro Agricultural Development Center" (ambacho kwa sasa kinaitwa Kituo cha Mafunzo ya Kilimo Kilimanjaro (KATC) "Kilimanjaro Agricultural Training Center".

Shughuli za ushirikiano sasa zimesambaa nchi nzima. JICA inatekeleza mipango miwili katika sekta ya kilimo, ambayo ni:

**i) Mpango wa kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga** "Program of Strengthening Rice Production" na

ii) Mpango wa kusaidia Sekta ya Maendeleo ya Kilimo "Program of Supporting Agricultural Sector Development Program" (ASDP).

i) Mpango wa kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga

Chini ya Mpango huu JICA imesaidia kusambaza teknolojia za kilimo cha mpunga kupitia miradi mbali mbali, yaani Mradi wa Kusaidia Kukuza Sekta ya Mpunga nchini Tanzania (TANRICE2), na Mradi wa Kujenga Uwezo kwa Wataalamu ili Kukuza Maendeleo ya Skimu za Umwagiliaji Chini ya Mipango ya Kilimo ya Wilaya Awamu ya II (TANCAID2), Mradi wa Kuendeleza Skimu za umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP), n.k.

**TANRICE: Ongezeko la uzalishaji wa mpunga na uboreshaji wa mavuno**

Kwa karibu nusu karne kuanzia mwaka 1974, JICA na Wizara ya Kilimo nchini Tanzania wamekuwa wakifanya kazi kwa pamoja katika eneo la kuendeleza zao la mpunga. Mfululizo wa miradi ya ushirikiano wa kitaalam imetekelezwa. Mipango mbali mbali ya mafunzo juu ya kilimo cha mpunga katika kilimo cha umwagiliaji na katika kilimo cha kutegemea mvua ilifanyika kwa maafisa ugani na wakulima kote nchini. Katika programu hizi za mafunzo, wakulima pia walijifunza mada zingine muhimu kama usimamizi wa mfumo wa umwagiliaji, jinsia, masoko, na usimamizi wa zana za mashine za kilimo

Jumla ya wakulima 5,235 walipata mafunzo katika miradi 44 ya umwagiliaji kupitia mradi wa ushirikiano wa kitaalam unaoitwa TANRICE (2007-2012). Baadaye, katika awamu ya 2 ya TANRICE 2 (2012-2019), teknolojia na ustadi huu ulisababisha kuongezeka kwa asilimia 40 ya uzalishaji wa mpunga chini ya kilimo cha kutegemea umwagiliaji, ongezeko la asilimia 50 chini ya kilimo cha kutegemea mvua cha mabondeni, na ongezeko la asilimia 140 chini ya kilimo cha kutegemea mvua katika nyanda za juu. Jumla ya wakulima 36,553 na maafisa ugani walipata mafunzo kupitia mradi huo wa TANRICE2.

Programu hiyo pia ilichangia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Mpunga Tanzania (NRDS) ambao ulilenga kuongeza uzalishaji wa mpunga nchini Tanzania kutoka tani 899,000 mnamo 2008 hadi tani 1,963,000 ifikapo 2018 chini ya mpango wa Coalition for African Rice Development (CARD). Lengo la awamu ya pili ya NRDS iliyozinduliwa mnamo mwaka 2019 ni kuhakikisha kuwa Taifa linajitosheleza katika uzalishaji wa mpunga, kuchangia utoshelevu wa mpunga katika eneo zima la Afrika, na kuwa kitovu cha masoko.

Kulingana na takwimu za Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) uzalishaji wa mpunga nchini Tanzania unakadiriwa kuongezeka mara 13, kutoka tani 223,000 (1974) hadi tani 3,016,695 (2018). Eneo la uzalishaji mpunga pia limeongezeka karibu mara 7, kutoka ha 163,000 (1974) hadi hekta 1,199,875 (2018). Aidha eneo la umwagiliaji limeongezeka mara 1.7 kutoka hekta 264,388 (2005/2006) hadi hekta 461,211 (2014/2015), kwa mujibu wa "Mpango kabambe wa Kitaifa wa Maendeleo ya Umwagiliaji" ulioundwa kwa utafiti wa pamoja kati ya Tume ya Umwagiliaji (NIRC) na JICA mnamo mwaka 2018. Ushirikiano wetu kupitia Programu ya Kuimarisha Uzalishaji wa Mpunga umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio yaliyotajwa hapo juu ya kuboresha maendeleo ya Mpunga na umwagiliaji.

**SSIDP & TANCAID2: Miongozo Yakinifu ya Maendeleo ya Miradi ya Umwagiliaji (CGL) kama msingi wa maendeleo ya umwagiliaji.**

JICA na Tume ya Umwagiliaji NIRC) wamekuwa wakiendeleza maendeleo ya mpango wa umwagiliaji shirikishi kwa kufuata mwongozo yakinifu. Katika mradi wa umwagiliaji (SSIDP), takriban Dola milioni 32 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu midogomidogo ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kazi za banio na mifereji ya umwagiliaji katika miradi ya umwagiliaji ipatayo 109 katika nchi nzima.

Kupitia hatua hizi, ongezeko la karibu hekari 20,000 za eneo lenye umwagiliaji linatarajiwa kupatikana. Mbali na uboreshaji wa miundombinu, jumla ya watu 9,921 wakiwemo wahandisi wa umwagiliaji na mafundi wa Tume ya Umwagiliaji na ofisi za wilaya, na wanachama wa vikundi vya umwagiliaji (IO) walipata mafunzo juu ya usimamizi sahihi wa mradi na uendeshaji na matengenezo (O&M) ya vifaa kama shughuli za mradi wa TANCAID2.

Mkulima mmoja katika mradi wa umwagiliaji wa Nyida huko Shinyanga alituambia kuwa baada ya mafunzo watu walianza kugawana maji kulingana na mpango wa usambazaji ambao ulitengenezwa



*Ukarabati shirikishi wa mfereji wa umwagiliaji.*



*Mfereji uliokamilika baada ya marekebisho.*

kwa msingi wa mwongozo uliotayarishwa na TANCAID2, badala ya kujichukulia maji kibinafsi. Aidha alisema kuwa kushiriki katika mgawanyo wa maji kumemfanya kuchangia kazi ya pamoja kama washiriki wa wanachama wa umwagiliaji (IO) katika utunzaji wa miundombinu. Pia mkulima mwingine katika mradi wa umwagiliaji wa Mkombilenga huko Iringa alituambia kuwa sasa ana uwezo wa kulipa ada ya shule kwa watoto wake. pia ameweza kujishughulisha na shughuli zingine kama vile utunzaji wa mifugo na shughuli za baa.

Washiriki wa chama cha umwagiliaji (IO) wakisakafia kitaalam mfereji wa umwagiliaji kwa msaada wa wafanyakazi wa wilaya na kanda.

ii) Mpango wa kusaidia Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo

Kupitia Programu hii, JICA ilipanua shughuli zake ili kujibu mahitaji ya kuimarisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa serikali (M&E) na kukuza uongezaji wa thamani na kilimo kinacholenga soko. JICA, pamoja na Wizara za Sekta ya Kilimo (ASLM) ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (TAMISEMI), inatekeleza miradi miwili.

- Mradi wa Ukuzaji wa Uwezo kwenye kukusanya takwimu mbalimbali Uchambuzi na Ripoti inayotegemea takwimu mbalimbali chini ya ASDP (ARDS)
- Mradi wa Uimarishaji wa Mpangilio wa Programu za Kilimo za wilaya (DADP) na Utekelezaji kupitia Matumizi ya mbinu ya SHEP (TANSHEP).

**ARDS:** Takwimu za kilimo zipo tayari kutumika katika kufanya maamuzi ya msingi katika sekta ya kilimo Tanzania



*(TANSHEP) Wakulima wakifanya Utafitii wa masoko*



*(TANSHEP) Wakulima wakisaidiwa kutengeneza kalenda ya uzalishaji kulenga kipindi chenye bei ya juu zaidi*

Kikosi kazi cha Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) katika Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) kimekuwa kikifanya kazi na Timu ya Mradi wa JICA. Mradi huu unakusudia kuboresha upatikanaji wa taarifa muhimu za kilimo kupitia Mfumo wa Takwimu za Njia ya Kilimo (ARDS) tangu mwaka 2008. Katika ARDS, taarifa zilizowekwa kisanifu kutoka kata hadi ngazi ya serikali kuu kupitia wilaya na mikoa zimeandaliwa. Takwimu hizo zimesajiliwa na kuhifadhiwa kwa pamoja kwenye Tovuti, ambayo ni programu iliyoandaliwa na kuendelezwa kwa matumizi yanayotokana na Tovuti iliyoundwa kwa kusudi hili maalum, na ripoti zinaweza kutolewa kwa urahisi kutoka kwa taarifa hiyo. Hatimaye ARDS inaruhusu watumiaji kupata, kuchakata na kusambaza taarifa za kilimo kupitia programu hii ya tovuti. Kwa kutumia mfumo huu, zaidi ya asilimia 90 ya taarifa za habari ya kilimo nchini kote zimewasilishwa kila mwezi tangu mwaka 2017. Kuzingatia kwamba kiwango cha uwasilishaji wa takwimu kama hiyo kilifikia asilimia 40mnamo 2015, ni maendeleo ya kustaajabisha katika miaka miwili. Sasa, Tovuti ya ARDS inafanya kazi nchini kote kulipo na muunganisho wa mtandao, na taarifa na ripoti zinazotokana na hiyo zinatumiwa vyema na Serikali

**TANSHEP: Kubadilisha kilimo kutoka "Kuzalisha na Kuuza" kuwa "Kuzalisha ili Kuuza"**

Tangu kuanzishwa kwakeJanuari mwaka 2019, TANSHEP imekuwa ikileta mbinu mpya za ugani, uwezeshaji na ukuzaji wa ukulima mdogomdogo wa mbogamboga (SHEP), kwa vikundi vya wakulima 56 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Wakati ambapo kwa pamoja wakulima wanatafuta soko la kile walichozalisha *("Kuzalisha na Kuuza")*, kwa njia ya SHEP, hufanya utafiti wa soko kabla ya kuanza uzalishaji, ambao huamua nini cha kuzalisha, vipi, na kulingana na mahitaji ya soko *(hiyo ni "Kuzalisha ili Kuuza")*. TANSHEP imeandaa mipango ya mafunzo ya kitaalam, juu ya utafiti wa soko, ujengaji wa wa biashara na wadau, na utunzaji wa kumbukumbu. Kwa kuwa haya ni majaribio yao ya kwanza, wakulima wanakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa (k.m mafuriko) na janga la ***COVID-19***.. Baadhi yao, kwa mfano, walicheleweshwa kupanda mbegu zao kwa mwezi mmoja, kisha wakaona bei kubwa za uuzaji wa kwanza lakini baadaye, kushuka kwa bei. Sasa wamekuwa makini zaidi na wanafuata kalenda ya upandaji mazao na kuyauza wakati bei ni nzuri. Wengine sasa wana uwezo wa kujadili na wanunuzi kadhaa, ili kuamua bei yenye faida kwao, kwa kutumia ufahamu wa utafiti wa soko waliopata kupitia mradi wa JICA.

Pamoja na maeneo muhimu ya ushirikiano yaliyoonyeshwa hapo juu, kazi za ujenzi wa Mradi wa Maendeleo ya soko la Samaki la Malindi huko Zanzibar ulianza mnamo mwaka 2019.

Kupitia msaada wa JICA, mkandarasi wa Kijapani alianza kurekebisha soko la samaki la Malindi na Vituo vya uuzaji wa samaki wa Malindi ili kuboresha utoaji wa huduma ili ziwe safi na salama zaidi kwa watumiaji, na hivyo kukuza upatikanaji wa samaki walio bora kwa watu wa Zanzibar. Vituo hivyo vinatarajiwa kubeba meli za uvuvi, kuleta ajira kwa watu kwenye sekta hiyo, na kuongeza mapato ya wadau katika minyororo ya thamani ya uvuvi, na hivyo kukuza uchumi wa Zanzibar.



*Kabla ya kuanza kazi za ujenzi (Desemba 2015)- Soko la Samaki Zanzibar*



*Baada ya kazi za ujenzi kuanza (Machi 2020)- Soko la Samaki Zanzibar*